Sisi Ni Wamoja

# MAONI YA WANANCHI KUHUSU SERIKALI YA UMOJA WA KITAIFA ZANZIBAR

## RIPOTI KUTOKANA NA MAJADILIANO KUPITIA MRADI WA SISI NI WAMOJA

## AGOSTI 2021 - APRILI 2022

Juwauza
Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar

## Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Shukrani | i |
| Muhutasari | ii |
| Orodha ya vifupisho | vi |
| Orodha ya Majadweli | vii |
| HISTORIA NA MAUDHUI | 1 |
| MBINU ZA USHIRIKISHAJI | 5 |
| MATOKEO MAKUU KUHUSIANA NA SUK | 7 |
| MAENEO YA VIPAUMBELE VYA KIJAMII NA KIMAENDELEO | 21 |
| MAPENDEKEZO NA MAONI YA WANANCHI | 33 |
| HITIMISHO | 42 |

**Shukrani**

Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA) inatoa shukrani zake za dhati kwa taasisi mbalimbali na watu waliochangia kwa mawazo na fedha kufanikisha mradi wa Sisi ni Wamoja, uliokusanya na kuwasilisha maoni ya wananchi kuhusiana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK). Mradi huu umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) ambapo ufadhili wake umeiwezesha JUWAUZA kuunda timu iliyofanikisha malengo ya mradi shirikishi wa Sisi ni Wamoja.

Aidha, tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa mashirikiano mazuri na msaada wa kitaalamu kutoka Taasisi ya Kitaifa ya Demokrasia (NDI), ambayo ilirahisha mchakato wa ushirikishaji wa wadau. Pia, tunaishukuru Bodi ya Wadhamini, Kamati Tendaji, washauri elekezi, wawezeshaji wa majadiliano ya kijamii, waandishi wa ripoti na watendaji wengine kwa jitihada zao zisizo ukomo kufanikisha mradi huu.

JUWAUZA inathamini mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hasa kutoka Ofisi ya Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ya Msajili wa Asasi za Kiraia, Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Makatibu Watendaji pamoja na Masheha ambao wametoa mchango mkubwa kufanikisha mradi huu. Kadhalika, JUWAUZA inashukuru ushiriki wa wananchi katika shughuli za kufanikisha mradi wa Sisi ni Wamoja.

Taarifa hii ni mchango wa dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watunga sera, vyama vya siasa, asasi za kiraia, taasisi za kidini na jamii kwa jumla. Taarifa hii itaisaidia Serikali katika ngazi zote kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi.

Taarifa inaainisha michango muhimu ya wadau katika kuunga mkono Zanzibar yenye amani na maendeleo, kama inavyotoa mapendekezo juu ya namna ya kujenga taifa imara lililoungana, na si lililokhitilafiana.

Kwa upande mwengine, JUWAUZA inachukua dhima kwa majumuisho, mapendekezo, makosa na dosari zilizomo katika taarifa hii.

**Muhutasari**

Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA) ambayo iliasisiwa mwezi Disemba 2008, ni taasisi isiyokuwa ya kiserikali na isiyotengeneza faida yenye lengo la kustawisha haki za wanawake na wasichana wenye ulemavu kupitia kujenga uelewa, mafunzo na kuwajengea uwezo. Taasisi hii inafanya kazi kwa ukaribu sana na taasisi nyengine za kiraia, serikali za mitaa na serikali kuu ya Zanzibar kwa kutetea haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu, hasa wanawake na wasichana, ikiamini kwamba watu hawa wanaweza kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za ufanyaji wa maamuzi.

Tangu kuasisiwa tena kwa siasa za vyama vingi mwaka 1992, mazingira ya kisiasa Zanzibar yamekuwa yakitawaliwa na mgawanyiko wa kisiasa uliosababishwa na hisia za kubaguliwa, kutengwa na kutowakiliswa kwa baadhi ya makundi ya watu katika jamii ya Zanzibar. Kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) mwaka 2010 kuliaminika kuwa ni mwarobaini kwa matatizo hayo, ambapo hilo lilifanyika katika kipindi cha mwaka 2010-2015. Hata hivyo, matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015 yalizima matumaini ya wananchi. Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilidumu kwa muda wa miaka 5 tu. Tangu kuingia madarakani kwa Dkt. Hussein Mwinyi mwaka 2020, kumekuwa na jitiada za ziada za kuhuisha SUK sambamba na kuimarisa mahusiano ya kijamii kwa maslahi ya taifa.

Kwa kutambua ukweli kwamba mfumo wa SUK umekumbana na changamoto za utekelezaji tangu kuanzishwa kwake mwaka 2010, na kwa kufahamu uzito wa kuimarisha na kudumisha SUK, JUWAUZA imebuni na kutekeleza mradi shirikishi ujulikanao kama Sisi ni Wamoja, ambao umetekelezwa kupitia majadilino na kukusanya maoni na matarajio ya wananchi ya kuimarisha mifumo na ufahamu wa SUK pamoja na hali ya maridhiano ya jamii katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Taarifa hii inawasilisha mambo muhimu yaliyopendekezwa na wananchi kupitia mijadala iliyofanywa na JUWAUZA katika kipindi cha Agosti 2021 hadi Aprili 2022 katika ngazi za kijamii na kitaifa. Katika utekelezaji wa mradi huu JUWAUZA ilifikia majimbo 25 (13 Unguja na 12 Pemba) na kuwashirikisha jumla ya wananchi 823; ambao kati yao 333 walikuwa wanawake na 490 wanaume, wakiwakilisha makundi mbalimbali ya jamii, taasisi na mashirika ya serikali ambao walipatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli (cluster sampling technique).

Kupitia utaratibu wa ushirikishaji, wananchi walipata fursa ya kupaza sauti zao kueleza maoni yao kwa ajili ya kuzingatiwa. Ufuatao ni muhtasari wa masuala yaliyoibuliwa:

Wananchi wameeleza uungaji wao mkono kwa uwepo wa SUK. Wananchi wanaamini umoja ni nguzo muhimu sana katika kulinda amani na utulivu nchini. Wameupongeza uongozi uliopo sasa chini ya Dkt. Hussein Mwinyi kwa jitihada za kufufua dhana ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na kuhamasisha amani na ushirikiano miongoni mwa wananchi wa Zanzibar. Hata hivyo, baadhi ya wananchi wanaamini kwamba utekelezaji wa SUK bado unakosa maamuzi ya dhati na utashi wa kisiasa ili kuleta mabadiliko.

Kuna kadhia nyingi zinazohusiana na taratibu za uajiri ambazo zimeelezwa kwa kurudiwa na wananchi zikiwemo upendeleo wa kidamu, upendeleo wa kichama, rushwa na ukandamizaji unaohusishwa na siasa unaofanywa na baadhi ya vyombo vya dola vinanvyohusihwa katika mchakato wa ajira za umma. Licha ya kuwepo kwa SUK, baadhi ya wananchi wanaamini kwamba bado kuna upendeleo unaotokana na mitazamo ya kisiasa katika utoaji wa fursa za ajira serikalini.

Wananchi wangependa kuona mfumo wa SUK unashuka katika ngazi zote za serikali ikiwemo Serikali za mikoa, wilaya na hata shehia. Wananchi wanaamini kwamba mfumo uliopo sasa, kama ulivyoelezwa katika katiba, umejikita tu katika ngazi ya juu kabisa ya Serikali na kuishia katika nafasi za uwaziri, na kutokuwepo katika ngazi nyengine za kitaifa.

Kwa nyakati mbalimbali wananchi wameelezea malalamiko yao kuhusiana na uhuru wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Wameielezea ZEC kuwa ipo katika milki ya chama tawala na hivyo kukosa uhuru na uwazi katika utendaji wake. Pia wananchi kwa mara kadhaa wameeleza kuwepo kwa udanganyifu wa hali ya juu katika upigaji kura wakati wa uchaguzi, changamoto wakati wa zoezi la usajili wapiga kura, hasa baadhi ya wapiga kura kucheleweshwa kwa makusudi kupatiwa vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi (ZanID). Kutokuwepo kwa fursa ya mgombea huru (asiyefungamana na chama chochote cha siasa), haja ya kuwepo program maalumu za kutoa elimu ya kupiga kura na madai ya kupinga kura ya mapema pia vilielezwa kama ni changamoto za mchakato huu.

Wananchi wanathamini jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali iliyopo madarakani za kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari na vyeti vya kuzaliwa. Hata hivyo, baadhi yao wameeleza kwamba bado kuna changamoto katika suala hili ambazo lazima zitatuliwe. Aidha, wananchi wameelezea tatizo la kuwepo kwa ubaguzi katika uhalali wa kupata ZanID na vyeti vya kuzaliwa katika ngazi ya shehia.

Uhaba wa huduma za afya na elimu, kutokuwepo kwa uelewa wa Sera ya Uchumi wa Buluu, kuongezeka kwa gharama za maisha na unyanyasaji wa kijinsia ni miongoni mwa masuala muhimu pia yaliyoibuliwa. Imani ya wananchi ni kwamba pamoja na kuwepo kwa utulivu wa kisiasa, serikali lazima ihakikishe upatikanaji wa maslahi ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

**Ufuatao ni muhtasari wa mapendekezo:**

Serikali ya Umoja wa Kitaifa inapaswa kuzingatia suala la ajira za serikali kutolewa kwa mujibu wa sifa za waombaji kadiri iwezekanavyo, na hilo lizingatiwe katika hatua zote za upokeaji maombi na uajiri. Tume ya Utumishi Serikalini inapaswa kuwa makini zaidi katika kuchunguza na kuchambua maombi ya ajira ili kuhakikisha inatenda haki. Na ili kurahisisha suala hili, kuna haja ya kuwa na mfumo wa kielektroniki wa uajiri utakaosimamia utaratibu wote wa uajiri hivyo kuleta ufanisi, uimara na usawa katika ajira za umma.

Taasisi za kiserikali na Asasi za kiraia zilizoshiriki katika majadiliano zilishauri kuwa kuna haja ya elimu zaidi kutolewa ili kuwasaidia wananchi kufahamu mfumo wa SUK, misingi yake, muundo wake pamoja na umuhimu wake. Wadau hao wanaamini kuwa ufahamu wa masuala hayo utasaidia wananchi kuepukana na mitazamo hasi ya kiitikadi na mihemko ya kisiasa au changamoto nyengine zinazoweza kurudisha nyuma hatua iliyofikiwa. Kwa mnasaba huo, serikali inapaswa kuwa makini zaidi kwa kutekeleza kivitendo matakwa ya SUK. Utashi wa kisiasa uliopo sasa hauna budi kuendelezwa ili kuielekeza SUK katika njia sahihi.

Aidha, vyama vya siasa vinavyounda SUK vinapaswa kufanya mashauriano ya ndani ili kuona jitihada ya kiasi gani inahitajika zaidi ili kuifikisha SUK katika ngazi za chini za serikali. Wadau wameeleza kuwa utashi wa kisiasa ndio changamoto

kubwa ambao huu uliopo sasa ni lazima uengwe engwe. Kutokana na umuhimu wake, vyama vinavyounda SUK vifikirie kutanua utendaji wa SUK katika ngazi zote za utawala wa serikali, kwa kuanzia na nafasi zisizokuwa na utata, na kumalizia zile zenye utata miongoni mwa vyama.

Wananchi walieleza kwamba uhai wa SUK unategemea sana uwezo wa ZEC kuendesha chaguzi kwa misingi ya haki. Kwa mantiki hiyo, upigaji kura ni lazima ufanyike kwa uhuru na uwazi; na ili kufikia hilo uhuru wa Tume ya Uchaguzi ni suala la msingi sana.

Kwa ajili ya kuanzisha mchakato wa suala hili, inapendekezwa kufanyike kongamano kubwa la kujadili mchakato wa marekebisho ya taratibu za uchaguzi kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Uzoefu kutoka vyombo vyengine vya kusimamia chaguzi pamoja na ushauri kutoka kwa wataalamu wa masuala ya uchaguzi pia vinaweza kutumika kuweka msukumo katika hili.

Wakala wa Usajili wa Masuala ya Kijamii (ZCSRA) inashauriwa kuhakikisha kwamba watu wote wanaostahiki wanapatiwa fursa ya kusajiliwa na kupatiwa ZanID, na kuanzishwe mfumo wa kidijitali ili kurahisisha zoezi hili.

JUWAUZA inaamini kwamba SUK itaimarika iwapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanyia kazi michango na mapendekezo haya kwa vitendo ili kuondoa changamoto zilizobainishwa na wananchi na kufikia matokeo yanayotarajiwa.

Tunaamini katika kuishi kwa amani na maelewano kwani pindi pakitokea ghasia hususan za kisiasa, wanawake na watu wenye ulemavu ndio wahanga wakubwa.

Kwa kutambua jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya awamu ya nane, JUWAUZA inawasilisha ripoti hii kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi, katika kushajiisha maelewano ya kijamii na kisiasa kwa kuimarisha utekelezji wa matakwa ya SUK.

## Orodha ya vifupisho

| Vifupisho | Maana |
|---|---|
| ACT | Alliance for Change and Transparency |
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| BLW | Baraza La Wawakilishi |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CUF | The Civic United Front |
| Dkt | Dokta |
| GBV | Gender-Based Violence |
| GS0 | Government Security Officer |
| ILO | International Labour Organization |
| JUWAUZA | Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar |
| Mh | Mheshimiwa |
| NDI | National Democratic Institute |
| NIDA | National Identification Authority |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| SUK | Serikali ya Umoja wa Kitaifa |
| USAID | United States Agency for International Development |
| ZanIDs | Zanzibar Residence Identity Card |
| ZCSRA | Zanzibar Civil Status Registration Authority |
| ZEC | Zanzibar Electoral Commission |

## Orodha ya Majadweli


| Nambari | Maelezo |
|---|---|
| **Jadweli 01** | Muhtasari wa changamoto zilizoibuliwa kuhusiana na mapungufu ya kimuundo ya SUK |
| **Jadweli 02** | Muhtasari wa masuala ya ajira yaliyoibuliwa |
| **Jadweli 03** | Muhtasari wa changamoto zilizoibuliwa kuhusiana na marekebisho ya taratibu za uchaguzi |
| **Jadweli 04** | Muhtasari wa Matokeo makuu yanayohusiana na SUK |
| **Jadweli 05** | Muhtasari wa changamoto zilizoibuliwa kuhusiana na masuala ya elimu |
| **Jadweli 06** | Muhtasari wa changamoto zilizoibuliwa kuhusiana na masuala ya afya |
| **Jadweli 07** | Muhtasari wa changamoto zilizoibuliwa kuhusiana na masuala ya uchumi wa buluu |
| **Jadweli 08** | Muhtasari wa vipaumbele vya masuala ya kijamii na kimaendeleo vilivyoibuliwa |

## HISTORIA NA MAUDHUI

### Muktadha wa kihistoria

Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) iliasisiwa mwaka 2010 kufuatia muwafaka baina ya vyama viwili vyenye ushindani mkubwa Zanzibar, baada ya majaribio mengi kushindwa kutokana na mivutano ya muda mrefu katika historia ya siasa ya Zanzibar, iliyosababisha kukosekana kwa amani na maelewano.

Kufuatia kura ya maoni ambayo asilimia 66.4% ya kura zilikubali mfumo wa SUK, Zanzibar ilianzisha mfumo huo tarehe 31 Julai 2010, na kupitisha mfumo mseto wa uongozi kwa njia ya kugawana madaraka. Hii ilipelekea mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kwa kuruhusu mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambao utekelezaji wake rasmi ulianza baada ya uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba mwaka 2010. SUK imekuwa ni kielelezo cha matumaini kwa Wazanzibari wengi, hasa wa upande wa upinzani, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia kutengwa na kubaguliwa katika jukwaa la siasa.

### Muongozo wa Kikatiba juu ya SUK

Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar inaendeshwa kwa mujibu wa Ibara ya 39-47 na Ibara ya 66 ya Katibaya Zanzibar kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010. Kwa mujibu wa Ibara ya 39 ya Katiba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na Makamo wawili wa Rais, ambao watajulikana kama Makamo wa Kwanza wa Rais, na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwa mujibu wa matakwa ya kikatiba, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anatakiwa kuteua Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais ndani ya kipindi cha siku saba baada ya kuapishwa kwake [Ibara 39 (2)].

Ibara ya 39 (3) ya Katiba inaeleza kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais atateuliwa iwapo atakuwa na sifa za kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na atateuliwa kwa mashauriano na chama kinachoshikilia nafasi ya pili kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi wa Rais.

Ibara ya 39 (3; i & ii) ya Katiba ya Zanzibar inaelekeza kuwa iwapo chama kinachoshikilia nafasi ya pili katika uchaguzi wa Rais kitakuwa na chini ya asilimia

10 ya kura, au iwapo Rais atasimama bila kupingwa, nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itakwenda kwa chama chochote kinachoshikilia nafasi ya pili kwa mujibu wa wingi wa viti vya majimbo katika Baraza la Wawakilishi. Msingi wa kipengele hiki ni kuimarisha demokrasia na utawala bora.

Vilevile, Ibara ya 42(1) ya Katiba inaeleza kuwa Rais, kwa makubaliano na Makamo wake wawili atateuwa mawaziri kutokana miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mawaziri watateuliwa kwa uwiano wa nafasi za viti vya majimbo kwa kila chama ndani ya Baraza la Wawakilishi. Ndani ya siku 14 baada ya kuteua Makamo wa Kwanza na wa Pili wa Rais, Rais atateua mawaziri.

**Utekelezaji wa kwanza wa muundo wa SUK**

Muundo wa SUK uliokubaliaka kikatiba ulianza kutekelezwa mwezi Novemba 2010 baada ya uchaguzi mkuu wa Zanzibar ambapo Dkt. Ali Mohamed Shein aliapishwa kuwa Rais wa Zanzibar. Marahemu Maalim Seif Sharif Hamad, ambae kwa wakati huo alikuwa Katibu Mkuu wa chama kikuu cha upinzani – CUF aliteuliwa kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali mpya, na Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Serikali hii iliundwa na wizara 16 (10 kutoka CCM na 6 kutoka CUF).

**Kusita kwa SUK**

Kusita kwa SUK kwa kiasi kikubwa kulisababishwa na mivutano ya mara kwa mara, ambapo mahusiano baina ya vyama viwili yalikuwa ya kimabishano zaidi kuliko ya kimashirikiano, hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu. Kwa mfano, katika awamu ya kwanza ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, mivutano baina ya vyama viwili vinavyounda SUK ilianza kujitokeza katika siku za mwisho kabla ya kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi kuelekea uchaguzi mkuu.

Tarehe 25 Oktoba 2015, Zanzibar na Tanzania Bara zilifanya uchaguzi mkuu wa 6 tangu kuanzishwa tena kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992. Licha ya uwepo wa SUK katika kipindi cha miaka 5 chini ya uongozi wa Dkt. Shein (2010 - 2015), vyama viwili vikuu vya siasa viliutazama uchaguzi wa 2015 kama ni lazima kushinda kutokana na kufungamana kwake na mwelekeo wa mabadiliko ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mabadiliko ambayo yalibeba mustakabali wa Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Msingi wa SUK ulipata majaribio baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015, ambapo ilionekana kuwa CUF ilijitangazia ushindi wa majimbo kadhaa Unguja, ambayo kabla yalikuwa ni ngome ya CCM. Jambo hili lilikiuka kanuni za ZEC ambazo zinaeleza kuwa ZEC pekee ndio yenye mamlaka ya kukusanya na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Mwenyekiti wa ZEC, ndugu Jecha Salim Jecha kwa maamuzi yake binafsi aliufuta uchaguzi mkuu tarehe 28 Oktoba kwa madai ya ***"kuharibika kwa uchaguzi na ukiukwaji wa kiwango kikubwa wa kanuni za uchaguzi".*** Uchaguzi wa marudio uliitishwa miezi mitatu baadae. Kutokana na kutoridhishwa na tukio hilo, CUF ilitangaza rasmi kugomea uchaguzi huo wa marudio, hivyo kuipa CCM ushindi mkubwa. Kutokuwepo kwa upinzani katika duru za siasa kumeifanya CCM kuunda serikali peke yake.

Maamuzi ya CCM kuunda Serikali bila ya upinzani yalipewa nguvu na Ibara ya 39 ya Katiba ya Zanzibar. Kwa msingi huo, ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ilibaki tupu, kwa kutokuwepo chama cha pili chenye sifa ya kutoa mwakilishi wa nafasi hiyo.

**Uongozi wa Dkt. Mwinyi na kuibuka tena kwa SUK**

Katika uchaguzi wa mwaka 2020, CCM ikiwakilishwa na Dkt. Hussein Mwinyi ilishinda nafasi ya urais kwa asilimia 78.2% dhidi ya mpinzani wake Maalim Seif Sharif Hamad ambae alipata asilimia 19% ya kura.

Akihutubia wananchi kwa mara ya kwanza baada ya kuapishwa katika Uwanja wa Amani tarehe 2 Novemba 2020, na kwa sauti ya maridhiano Dkt. Mwinyi aliweka bayana utayari wake kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba na kuleza wazi kuwa:

> *"Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wote bila ya kujali mirengo yao ya kisiasa; nawaahidi kwamba niko tayari kuyafanyia kazi maridhiano"*

Baada ya mashauriano ya ndani ya chama, ACT Wazalendo, chama kinachoongoza upinzani Zanzibar kilikubali kuingia na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Rais Mwinyi ameunda SUK inayoonesha matumaini mazuri na amewateua viongozi wa juu wa ACT Wazalendo katika Baraza lake la Mawaziri ambao ni Mhe. Nassor

Ahmed Mazrui – Waziri wa Afya; na Mhe. Omar Said Shabaan – Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Mawaziri wote wawili ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hivyo uteuzi wao katika nafasi ya uwaziri unaendana na matakwa ya Katiba ya Zanzibar Ibara ya 9 (3), ambayo inasisitiza umuhimu wa SUK kama msingi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dkt. Mwinyi amekuwa akitumia majukwaa mbalimbali ikiwemo sala za Ijumaa katika misikiti mbalimbali Unguja na Pemba kuhubiri umuhimu wa umoja na mshikamano. Mwenendo huu umepata mapokezi mazuri kwa wananchi wengi na kuonekana kama ni ishara njema ya kuponesha majeraha ya kisiasa na kufungua ukurasa mpya wa matumaini, ushirikiano na kuvumiliana.

**Ushiriki wa wananchi katika SUK**

Katika kuunga mkono jitihada za Serikali chini ya uongozi wa Dkt. Mwinyi, JUWAUZA imeendesha majadiliano na midahalo ya wananchi ili kukusanya mawazo ya wananchi kutoka maeneo yote (mjini na vijijini) na kuchangia uimarishaji wa umoja wa kitaifa na mshikamano, kuhuisha mafungamano ya kijamii na ushirikishwaji jumuishi wa kisiasa nchini.

Lengo kubwa la mradi huu uliojikita kwa wananchi ni kuwashirikisha wananchi katika ngazi za chini za jamii na kuwahamasisha katika kujenga SUK kwa mtazamo wa kushajiisha maridhiano ya kijamii na kujenga jukwaa la kukusanya mawazo na mapendekezo ya wananchi kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi, watunga sera na wadau wengine wenye mamlaka ya uendeshaji na utekelezaji wa SUK, hasa katika muktadha wa uboreshaji wa mazingira ya kisiasa na chaguzi.

## MBINU ZA USHIRIKISHAJI

Ili kuhakikisha matokeo mazuri ya mradi huu, njia kadhaa zilitumika kuandaa majadiliano kama inavyoainishwa hapa chini:

### Mbinu zilizotumika kukusanya maoni ya wananchi

Midahalo na majadiliano ilifanyika kama mbinu ya kukusanya maoni ya wananchi juu ya utekelezaji wa SUK. JUWAUZA iliendesha jumla ya majadiliano 38 ya kijamii (yakiwemo 6 ya vijana na 6 kwa wanawake pekee), yaliyoendeshwa katika majimbo 25 kati ya majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo majimbo 13 yalikuwa kwa upande wa Unguja na majimbo 12 kwa upande wa Pemba. Aidha, majadiliano mengine mawili ya ziada yaliyohuhsisha Taasisi za kiserikali na Asasi za Kiraia (AzaKi) yalifanyika kwa upande wa Unguja. Vigezo vilivyotumika kuchagua majimbo ni pamoja na mtazamo wa kijiografia, mchanganyiko wa kisiasa, pamoja na usawa baina ya mjini na vijijini.

Majimbo 13 yaliyofikiwa kwa upande wa Unguja ni pamoja na Tumbatu, Tunguu, Mwanakwerekwe, Bububu, Nungwi, Mtoni, Dimani, Malindi, Kijini, Chaani, Bubwini, Chwaka, and Paje; wakati kwa upande wa Pemba majimbo 12 ni Chake-Chake, Wete, Micheweni, Mtambile, Konde, Mkoani, Chonga, Ziwani, Wingwi, Chambani, Kojani and Pandani.

Kwa ujumla majadiliano yote 40 yalifikia idadi ya watu 823 wakiwakilisha makundi mbalimbali ya kijamii, ambapo wadau 333 walikuwa wanawake na 490 wanaume. Kila mjadala ulihusisha kati ya watu 20 hadi 25 ambao walichanguliwa kwa vigezo vya umri, jinsia na uwakilishi wa makundi mbalimbali wakiwemo wanasiasa.

Majadiliano yaliwakusanya wadau wenye kuwakilisha makundi ya watu wenye ulemavu, vijana, wanawake, jumuiya za wavuvi, wakulima, viongozi wa dini, wazee, vikundi vya wafanyabiashara wadogo wadogo (bodaboda na mama lishe), vyama vya siasa (CCM, ACT- Wazalendo na CUF), ofisi za masheha, wasaidizi wa sheria na walimu wa madrasa na skuli.

Mchakato wa kushajiisha ushiriki wa wananchi ulisimamiwa na mratibu wa ushirikishaji jamii kwa kusaidiana na wasaidizi wa sheria pamoja na msaada mkubwa kutoka kwa masheha wa shehia husika.

**Kuibua maoni ya wananchi katika utekelezaji wa SUK**

Majadiliano yote ya kijamii yaliendeshwa na wawezeshaji wenye utaalamu kwa lengo kuu la kupata michango kutoka kwa washiriki juu ya SUK kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

- Uelewa wa wananchi kuhusiana na maana ya SUK kwa mtazamo wao

- Mitazamo ya wananchi juu ya hali ya maridhiano, iwapo ni hatua chanya au hasi iliyofikiwa;

- Matazamio na matarajio ya Wazanzibari juu ya utekelezaji wa SUK kwa kuboresha mifumo ya utawala;

- Ufahamu wa pamoja wa wananchi kuhusu SUK na hasa nafasi yake katika kuimarisha mtangamano wa amani; na

- Nafasi na uwezo wa SUK katika maridhiano ya kisiasa kwa wananchi wa Unguja na Pemba, ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa katika mivutano ya kisiasa ambayo baadhi ya wakati huhusisha matumizi ya nguvu.

Matokeo yote yaliyopatikana katika mradi huu yamegawanywa katika makundi matatu;

i. Matokeo makuu kuhusiana na SUK;
ii. Masuala ya vipaumbele ya kijamii na kimaendeleo;
iii. Mapendekezo na Maoni ya Wananchi.

## MATOKEO MAKUU KUHUSIANA NA SUK

Katika majadiliano yote, wananchi walieleza mitazamo yao kuhusiana na maridhiano ya kisiasa katika uendeshaji wa SUK ambayo kama haikuangaliwa kwa tahadhari inaweza kuzorotesha jitihada na utendaji wa SUK. Yafuatayo ni matokeo makuu kuhusiana na SUK kama yalivyokusanywa kupitia majadiliano:

1. **Kasoro za kimuundo wa SUK/ kuishusha SUK hadi ngazi za chini za serikali**

Suala la muundo wa SUK limezungumzwa mara kadhaa katika majadiliano. Wananchi wengi wanaamini kwamba muundo uliopo sasa wa SUK kama ulivyowekwa katika katiba umejikita katika nafasi za juu tu za serikali na kuishia katika nafasi za uwaziri; hivyo kufanya SUK ionekane katika ngazi ya kitaifa tu. Kwa mfano, wananchi wa Fukuchani wameeleza hamu yao ya kutaka kuona mfumo wa SUK unashuka kutoka ngazi za juu hadi ngazi ya shehia.

*"Kama chama kimepata wastani unaotakiwa kushiriki kuunda serikali maana yake watu wamekikubali. Italeta maana nzuri ikiwa serikali itakua na uwakilishi katika ngazi zote sio tu baraza la mawaziri bali mpaka katika uteuzi wa Masheha uzingatie uwepo wa vyama vyote''*

Imeelezwa na mwananchi mmoja akiwakilisha walimu wa skuli kuashiria kwamba iwapo chama kitapata asilimia ya kutosha ya kura kuunda serikali, inamaanisha kuwa wananchi wamekiridhia chama hicho. Ili kuipa SUK maana zaidi na kuifanya kuwa wakilishi, ngazi zote za ufanyaji maamuzi, kuanzia baraza la mawaziri hadi shehia lazima zionekane katika mfumo wa SUK. Hili litaimarisha maelewano katika jamii na kupuguza upendeleo.

Hisia kama hizo zimeelezwa pia kupitia majadiliano ya wananchi katika maeneo ya Kisauni, Tomondo, Bwejuu, na Kwagowa. Imeelezwa kuwa kutokuwepo kwa uwakilishi katika ngazi ya chini ya serikali kunapelekea kukosekana kwa mrejesho kuhusiana na utendaji wa SUK, na kwamba kukosekana kwa mrejesho kunawakosesha wananchi msingi wa kutathmini ufanisi wa Serikali, na kwa mantiki hiyo wanahisi kuwa wametengwa.

Katika vipindi kadhaa vya majadiliano, wananchi walidai haja ya kufanyika marekebiso mengine ya katiba ili kutanua wigo wa SUK na kuifikisha katika ngazi ya shehia. Wananchi wamesisitiza kwamba ofisi za sheha na kamati za shehia zinapaswa kujumuisha wajumbe kutoka upinzani ili kuhakikisha kwamba dhana ya SUK inarasimishwa na inahuishwa katika mfumo wa serikali za mitaa.

Aidha, imependekezwa kwamba mamlaka za serikali za mikoa na wilaya zigawiwe miongoni mwa vyama vikubwa, na kwamba wajumbe kutoka upinzani wateuliwe kushika nafasi za ukuu wa mikoa na wilaya. Hii itapunguza misuguano inayotokana na kuchukizwa na ubaguzi miongoni mwa wananchi, na itaweka mgawanyo mzuri wa madaraka katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu.

*Jadweli 01: Muhtasari wa hoja zilizoibuliwa kuhusu mapungufu ya kimuundo ya SUK*

| **Nambari** | **Hoja zilizoibuliwa** |
|---|---|
| **i.** | SUK ni serikali inayoonekana katika ngazi ya juu tu, katika nafasi za urais na wizara |
| **ii.** | Kutanua wigo wa SUK hadi ngazi ya shehia na kamati zake. |
| **iii.** | Kutanua wigo wa SUK hadi katika nafasi za ukuu wa wilaya na mikoa na kuteua wajumbe kutoka upinzani kushikilia baadhi ya nafasi hizo. |
| **iv.** | Vyama vingine vyenye usajili wa kudumu vishirikishwe katika kuunda SUK |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

### 2. *Upendeleo, rushwa, na upendeleo wa kichama katika fursa za ajira za umma.*

Wananchi wameeleza hisia zao kuhusiana na kile wanachokiona kuwa ni upendeleo unaotokana na mrengo wa kichama katika suala la ajira za umma. Wakati wa majadiliano ya Uvivini, kwa mfano, mwanafunzi wa chuo kikuu aliyehitimu hivi karibuni alieleza kuwa hali ni mbaya katika mchakato wa ajira za serikali ambao unaonekana kugubikwa na upendeleo. Vijana wengi walioshiriki majadiliano haya walieleza kuwa ni vigumu kupata ajira za serikali isipokuwa tu kama mtu atakuwa na kadi ya uwanachama wa CCM au jamaa wa karibu anaefanya kazi serikalini ambae anaweza kumsaidia mtu wake kupata ajira.

> *"...Ni vigumu kupata kazi, lazima uwe na kadi ya chama au jamaa yako yupo serikalini ndio akusaidie, bila hivyo hamna kitu"*

Vijana katika majadiliano ya Mtakuja, Mwanyanya, na Kangagani walitoa malalamiko kama hayo kuhusu ugumu wa kupata ajira za serikali, hasa ikiwa mtu anahusishwa na chama cha upinzani. Wamesisitiza haja ya kuwa na mshikamano na kutaka kumalizwa kwa tofauti za kisiasa. Vijana walibainisha kuwa mchakato wa ajira uzingatie uwezo zaidi kuliko ufuasi wa kikabila na mitazamo ya kisiasa ili kupata watendaji wazuri.

Hivyo hivyo, GSO imelalamikiwa kwa kuangalia zaidi ufuasi wa kisiasa wakati wa uchunguzi wa waombaji wa ajira serikalini. Kijana mmoja katika majadiliano ya Chwaka alieleza kuwa GSO imekuwa kikwazo kikubwa kwa ajira za serikalini kwa miaka mingi. Alieleza kuwa iwapo mhusika au wazazi wake wanahusiana na chama cha upinzani basi atatolewa tu hata kama ana sifa zote kwa nafasi husika.

Ili kupunguza hisia za "Umimi na Usisi" wananchi waliomba GSO iwe inaangalia uwezo wa mtu katika kuchunguza maombi ya ajira.

Wananchi wa Bwejuu na Makoongwe wanaamini kuwa rushwa kwa kiwango kikubwa inakwaza ajira za umma. Wameeleza kuwa watu wenye wasaa mzuri wa kifedha au wanaoweza kutoa rushwa wanaweza kwa haraka sana kupata ajira hata kama hawana sifa za kazi hiyo.

Imani kubwa iliyopo miongoni mwa Wazanzibari ni kuwa upatikanaji wa ajira serikalini unategemea sana kujuana baina ya mtu na mtu. Mwananchi mmoja wa Msuka Mashariki alieleza kuwa wale wenye jamaa zao serikalini wana nafasi kubwa

ya kupata taarifa za ajira na wanaweza kusaidiwa pia kupata fursa zenyewe kwa njia ya upendeleo.

Wananchi katika majadiliano ya Kilindi walieleza kuwa ajira za umma hazijagawanywa kwa usawa kati ya maeneo ya mijini na vijijini. Wanaona kuwa idadi ya fursa zinazotolewa vijijini haitoshi kukidhi mahitaji; na kwamba fursa nyingi zinatolewa mijini, na maeneo mengi ya vijijini yana watumishi wachache wa umma. Wakati huohuo, wananchi wengine katika majadiliano hayo walilalamikia tabia ya watumishi wa umma kuhama mara tu baada ya kupangiwa kazi maeneo ya vijijini.

Wananchi wengi katika midahalo ya vijijini Unguja na Pemba waliiomba serikali kushughulikia suala la kutokuwepo uwiano wa watumishi wa umma katika maeneo ya vijijini. Baadhi ya watumishi wa umma walioajiriwa katika maeneo ya vijijini hutumia ajira zao hizo kama mpito tu, na hatimaye kuhamia maeneo mengine, hasa mijini, na kuacha jamii za vijijini na pengo kubwa la wafanyakazi.

*Jadweli 02: Muhtasari wa hoja za ajira zilizoibuliwa*

| **Nambari** | **Hoja zilizoibuliwa** |
| --- | --- |
| **i.** | Upendeleo wa kichama katika fursa za ajira za umma |
| **ii.** | Uonevu wa kisiasa unaofanywa na GSO katika mchakato wa ajira za umma |
| **iii.** | Rushwa katika ajira za umma |
| **iv.** | Upendeleo na uhusiano wa kibinafsi katika ajira ya umma |
| **v.** | Kutokuwepo kwa uwiano wa mgao wa watumishi wa umma vijijini |
| **vi.** | Unyanyasaji wa wenyeji unaofanywa na wawekezaji wa hoteli |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

### *3. Marekebisho ya taratibu za uchaguzi na uhuru wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC)*

Katika mijadala mbalimbali, wananchi wamehoji kuhusu uhuru wa ZEC, wakiituhumu kuwa ni milki ya chama tawala na kukosa uhuru na uwazi, hasa kipindi cha uchaguzi. Katika majadiliano ya Makadara na Mwanyanya wananchi walitilia shaka uhuru wa ZEC kwa kubainisha kwamba maamuzi yake yamekuwa yakichochewa na kuchezewa. Wananchi waliongeza kuwa kukosekana kwa uwazi kwa tume hiyo kumesababisha sintofahamu nyingi kati ya vyama vikuu hasa wakati wa uchaguzi. Chini ya muundo wa sasa wa ZEC, chaguzi haziwezi kuwa za haki, kwa mujibu wa raia wa Makadara anayewakilisha watu wenye ulemavu. Iwapo tume itakuwa huru, basi itapunguza mivutano ya kisiasa na madai ya udanganyifu wa uchaguzi.

> *‘‘kama tume ikiwa huru itasaidia kupunguza mvutano na madai ya udanganyifu wa uchaguzi, uchaguzi huu wa Zanzibar hautoacha kuwa na dosari kama ZEC ndio ileile’’*

Kwa mujibu wa wananchi, Chaguzi ndani ya Zanzibar ndio chanzo kikuu cha mivutano ya kijamii na kisiasa; kwa hivyo, uwezekano wa kudumu muda mrefu kwa SUK utategemea kwa kiasi kikubwa nia njema ya kuendesha chaguzi huru na za haki. SUK ilikaribia kusambaratika mwaka 2015 kwa sababu zile zile za upendeleo wa ZEC na madai ya udanganyifu wa uchaguzi.

Iwapo hatua stahiki hazitachukuliwa kudhibiti changamoto zilizotajwa hapo juu, hatua zote zilizofikiwa hapo awali zinaweza kupotea, SUK ni matokeo ya chaguzi zilizokuwa zikishindaniwa hapo awali. Uhai wake unategemea chaguzi zilizo halali na zisizo na upendeleo.

Katika majadiliano mengi ya Unguja na Pemba wadau walidai kuwa kuna mtindo unaojirudia mara kwa mara wa udanganyifu mkubwa wa kura wakati wa uchaguzi, unaochangia kupingwa kwa matokeo ya uchaguzi. Upigaji kura unapaswa kufanyika katika mazingira huru na ya uwazi, kama walivyopendekeza, ili kupunguza malalamiko kuhusu matokeo ya uchaguzi. Mwananchi mmoja anayeiwakilisha ACT Wazalendo alidai kuwa, akiwa mwangalizi wa chama katika uchaguzi wa mwaka

2020, alizuiwa kusimamia zoezi la upigaji kura hadi matokeo yalipotangazwa; hali hii inazua wasiwasi kuhusu uhalisi wa matokeo, na akahimiza kuwepo kwa mchakato wa uchaguzi ulio wazi.

Wakati wa midahalo, wananchi waliibua wasiwasi kuhusiana na changamoto za usajili wa wapiga kura. Baadhi waliripoti kuwa upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa na ZanID umecheleweshwa makusudi, hivyo kufanya vigumu kwao kujiandikisha kupiga kura.

Wananchi walisisitiza umuhimu wa elimu ya mpiga kura. Wakati uchaguzi unapokaribia nchini kote, ZEC inapaswa kutekeleza programu za elimu ya wapigakura ili wananchi wajue mahitaji ya msingi ya sheria na kanuni za uchaguzi. Hii pia itasaidia kuzuia majibizano yasiyo ya lazima kati ya raia na vikosi vya usalama.

Aidha wananchi hao walieleza kuwa Baraza la Wawakilishi lazima lifanyie marekebisho Kanuni za Uchaguzi za Zanzibar haraka na kuondosha kura ya mapema. Washiriki walidai kuwa kanuni ya kura ya mapema ndiyo ilichochea sintofahamu katika uchaguzi uliopita wa 2020, na walipendekeza zoezi la upigaji kura lifanyike kwa siku moja, kama ilivyo kwa Tanzania Bara, ili kuondosha hofu ya uchaguzi usio wa haki. Wananchi wanaamini kwamba iwapo mamlaka hiyo itashughulikia masuala haya ipasavyo, itachangia kupatikana kwa amani, maelewano, na SUK itakayodumu muda mrefu.

*Jadweli 03: Muhtasari wa hoja zilizoibuliwa kuhusu marekebisho ya taratibu za uchaguzi*

| Nambari | Hoja zilizoibuliwa |
|---|---|
| **i.** | Uhuru wa ZEC |
| **ii.** | Changamoto wakati wa zoezi la uandikishaji wapiga kura |
| **iii.** | Uwazi wakati wa kupiga kura |
| **iv.** | Kuondoshwa kwa kura ya mapema |
| **v.** | Haja ya elimu ya mpiga kura |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

### 4. *Kunyimwa haki ya kupata ZanID/ Vyeti vya kuzaliwa*

Wananchi wengi walikiri kuwa serikali imefanya mabadiliko makubwa ambayo yamepunguza kwa kiasi kikubwa vikwazo vya kupata ZanID na vyeti vya kuzaliwa. Majadiliano mengi yalizungumzia haja ya kuwa na ZanID na vyeti vya kuzaliwa hata baada ya uchaguzi. Hata hivyo, ilielezwa kuwa karibu katika kila Shehia bado kuna vikwazo ambavyo lazima vitatuliwe. Katika majadiliano hayo, wananchi walieleza wasiwasi wao kuhusu ubaguzi wanaokumbana nao kutoka kwa baadhi ya masheha wakati wanapoomba kihalali vitambulisho vya Mzanzibari na vyeti vya kuzaliwa.

Mwananchi kutoka Kangagani anaewakilisha kikundi cha vijana alisema, "Nimesubiri karibu miaka miwili tangu nilipoomba ZanID yangu, na sijawahi kupata jibu la kuridhisha nilipouliza kuhusu hatua iliyofikia."

*“niliwahi kukaa yapata miaka miwili, nasubiri kitambulisho, kila nikienda kuulizia kama kipo tayari, naona sielewi’’*

Mwananchi mmoja katika mdahalo wa Bandakuu alielezea muktadha unaofanana na huo kwa kusema, "Wakati fulani nilishindwa kuanza mchakato wa maombi ya ZanID kwa sababu Sheha alidai mimi sio wa hapa. Nilizaliwa na kukulia hapa miaka 25 iliyopita; iweje Sheha kudai kuwa hanitambui?"

Wananchi kutoka Ole, Tomondo na Jongowe walipendekeza kuwa Wakala wa Usajili wa Masuala ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) isambae katika mikoa na taarifa za upatikanaji wa hati hizo muhimu (vyeti vya kuzaliwa na ZanID) zitolewe kwa wananchi wote wanaostahiki, bila kujali makundi yao au mrengo wa kisiasa.

### 5. *Kubaguliwa na kutengwa kisiasa*

Kutokana na imani zao za kisiasa, wananchi walionesha hisia za kubaguliwa na kutengwa. Katika midahalo ya Jongowe na Uvivini, wananchi walisisitiza kuwa ili Serikali ya Umoja wa Kitaifa ifanye kazi kwa ufanisi, ni lazima serikali igawanye miradi ya maendeleo kwa usawa bila kujali mirengo ya kisiasa au kiitikadi.

Wananchi wa Jongowe walieleza kuwa shehia yao imetengwa na shehia nyingine tatu za Tumbatu kwa muda mrefu kwa sababu ni shehia pekee ndani ya visiwa vya Tumbatu inayounga mkono upinzani.

Kuhusu kukosekana kwa uendelezaji wa miundombinu katika shehia zao, wananchi wa Makangale, Maziwa Ng'ombe, na Uzi Ng'ambwa walitoa maoni yanayofanana. Kwanza, kuna dhana kwamba ugawaji wa mipango ya kimaendeleo inapendelea maeneo ya mijini kuliko jamii za vijijini.

Wananchi katika mdahalo wa Maziwa Ng'ombe walionyesha kwa uwazi kutengwa kwa kueleza kuwa hawaoni tofauti kati ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Serikali zilizopita kabla ya mchakato wa maridhiano kuhusu faida za kimaendeleo.

Wananchi katika midahalo mingi kisiwani Pemba walieleza kuwa ili kudumisha maelewano ya kisiasa ni lazima kwanza serikali ioneshe umoja wake kwa vitendo kwa kutenga miradi mbali mbali ya kimaendeleo kwa mikoa tofauti kulingana na mahitaji yao.

Aidha, wananchi katika midahalo mingi ya Unguja walipendekeza kuwa maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji yasipuuzwe wakati wa kupanga mikakati ya maendeleo ili kukabiliana na tofauti za kijamii na kiuchumi kati ya jamii za vijijini na mijini.

### *6. Umuhimu wa SUK na kuimarisha mtangamano wa kisiasa.*

Wananchi wengi wameonesha uungaji mkono wao usioyumba kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Bila ya umoja, utulivu wa kisiasa na kuishi pamoja miongoni mwa Wazanzibari vinaweza kutoweka, kama walivyoeleza baadhi yao. Wananchi walipongeza juhudi za Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi za kuendeleza ajenda ya maendeleo ya Zanzibar na Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Wakati wa majadiliano ya Matemwe, wananchi walieleza kuwa uwepo wa SUK umesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa mivutano yao ya kijamii ya hapo kabla, ambapo ilifikia mahali hakuna mtu aliyehudhuria mazishi au kuzungumza na mwenzake, na hata ndugu waligombana kwa sababu ya siasa. Katika midahalo ya Wingwi Mapofu, Mgagadu, Mkanyageni, na Kilindi wananchi walitoa ushahidi wao kwa nyakati tofauti kuwa hawakuweza kuhudhuria shughuli za mazishi siku za nyuma kwa sababu ya tofauti za kisiasa.

Amani ni muhimu katika kuleta maendeleo, na wananchi kutoka Sizini wameeleza kuwa serikali inaweza kutumia utaratibu wa kisheria wa SUK kuweka mazingira ya amani yatakayovutia wawekezaji wengi wa kigeni. Hivyo, kuwepo kwa SUK ni mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi kwa sababu watu wanapata fursa ya kushirikiana na kubadilishana mawazo wakati wa kujadili masuala ya kimaendeleo.

Kwa ujumla, katika kuunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hoja zifuatazo ziliibuliwa:

i. ***Kurudisha mfumo wa wazee kushiriki katika vikao na kujenga upatanishi katika ngazi za chini***

Katika majadiliano mengi yaliyofanyika maeneo ya vijijini na katika visiwa vidogovidogo kama vile Uzi na Micheweni, wananchi walipendekeza kuundwa kwa kamati za kijamii za wazee ambazo majukumu yake ya msingi yatakuwa ni kuimarisha mahusiano na kukuza maridhiano na mshikamano. Wananchi walisifu muundo wa kijadi uliokuwepo zamani, lakini ambao haukuweza kufanya kazi kutokana na mgawanyiko mkubwa wa kisiasa na kuundwa kwa kamati za shehia.

ii. ***Kubadilishana mikutano ya kisiasa katika ngome za vyama tofauti***

Wakati wa majadiliano yaliyofanyika Bandakuu, Gulioni, Sharifu Msa, Tomondo, na Gomani, wananchi walipendekeza kuwa Rais na Makamu wake wawili wafanye mikutano ya kisiasa na ya hadhara ili kuongeza uelewa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa wananchi. Rais na Makamu wa Pili wa Rais wanapaswa kufanya mikutano ya hadhara katika ngome za ACT-Wazalendo, kama ambavyo Makamu wa Kwanza wa Rais atafanya hivyo katika ngome za CCM, ili kurudisha mahusiano mazuri katika jamii. Kwa msingi huo, wananchi walimtaka Rais na Makamu wake kutoa mrejesho wa utendaji kazi wa SUK kupitia misikiti na makanisa na mikutano ya hadhara.

Mwananchi wa Tomondo aliyewakilisha viongozi wa dini alieleza kuwa viongozi wakuu wa serikali wanapaswa wasiwe wanatembelea misikiti tu kwa ajili ya kuhamasisha amani, bali wawe na mipango ya kutembelea makanisa pia kwani wao ni viongozi wa kiroho wa watu wa madhehebu na dini mbalimbali.

Wananchi wa Bandakuu, Gulioni, Sharifu Msa, Tomondo, Kojani, na Gomani walimpongeza Rais kwa kuwa na ziara za mazungumzo na wananchi wa mjini. Hata hivyo, walihitaji fursa sawa ya kukutana na Rais kwa upande wa vijijini ili kupeana taarifa za mambo yanayoendelea nchini. Walisema kuwa wana imani na uwezo wa Rais katika uongozi.

### iii. *Kuunda chombo huru cha kusimamia utendaji wa SUK*

Katika midahalo iliyofanyika Gomani, Makoongwe, Kojani na Ijitimai, wananchi walieleza hamu yao ya kutaka Rais Mwinyi aunde tume huru itakayoripoti kwake itakayojumuisha wataalamu wasioegemea upande wowote wa kisiasa, na ambao wataendeleza maridhiano na kuendeleza umoja wa kitaifa. Wananchi pia walipendekeza kuanzishwa kwa majukwaa ya kijamii yatakayofanya kazi ya maridhiano, kuponya majeraha ya kisiasa na kujenga imani miongoni mwa Wazanzibari. Majukwaa hayo yajumuishe viongozi wa dini na taasisi zisizokuwa za serikali kutoka maeneo tofauti.

### iv. *Vyama vingi zaidi vishirikishwe katika SUK*

Wananchi wameonesha hamu ya kuendelea kwa SUK na kuimarishwa misingi yake katika Katiba. Kwa mfano, wananchi wa Makangale walisisitiza umuhimu wa kutanua wigo wa SUK kwenye Katiba ili kuona uwezekano wa vyama vingine kushiriki katika kuunda serikali.

### v. *Kuanzisha warsha nyingi zaidi za uhamasishaji*

Wananchi katika midahalo mingi Unguja na Pemba walipendekeza haja ya kutolewa elimu ya uraia ili kuwapatia uelewa mzuri zaidi wa SUK. Kwa mfano, wananchi kutoka Uvivini na Jongowe walidai kufanyike warsha za uhamasishaji na wananchi wa Tumbatu, lakini hasa na vyama vya siasa vinavyounda SUK hivi sasa. Elimu hiyo inapaswa kusisitiza maridhiano na uelewa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na malengo yake.

## 7. Uelewa mdogo kuhusu SUK

Wananchi wachache walionesha uelewa na maudhui ya msingi wa SUK, ingawa baadhi yao walionesha uelewa mdogo wa dhana hiyo, na walio wengi hawaelewi kikamilifu SUK. Kwa kuwa SUK inagusa pande zote za jamii ya Zanzibar, kuna haja ya kutolewa kwa elimu ya uraia, hasa kwa jamii za vijijini na ngazi za chini ambako baadhi ya watu bado wana chuki za kisiasa.

Wananchi walioshiriki majadiliano ya Sizini, Marumbi, na Mkanyageni hawakuwa wakifahamu kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilitokana na kura ya maoni iliyofanyika mwaka 2010. Pia, hawakuwa wakijua kuwa matokeo ya kura za maoni ndiyo yaliyopelekea mabadiliko ya 10 ya Katiba na kuruhusu muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wananchi hawa hawakuwa na uhakika kama SUK ipo kwa mujibu wa Katiba.

Wakati wa mdahalo wa Makoongwe, wananchi walisema kuwa kuanzishwa kwa SUK kunaongeza tu gharama za uendeshaji wa serikali. Wanaamini hakuna tofauti kati ya serikali kabla ya SUK na baada ya kuanzishwa kwa SUK; na kwamba vyama vingine vinapaswa kuondolewa ili kulinda amani ya muda mrefu na kuepuka migogoro ya kisiasa. Wananchi wamependekeza kurejea katika mfumo wa chama kimoja.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara kadhaa ilitamkwa kama Serikali ya Umoja wa kimataifa na wananchi kadhaa. Wakati wa kuwasilisha michango yao, wananchi katika midahalo ya Matemwe, Bwejuu, Ngwachani, Sizini na Msuka Mashariki walitumia maneno haya mara kwa mara kwa kuyabadilisha. Ingawa maneno haya kimsingi yana maana mbili tofauti, matumizi ya mara kwa mara ya istilahi hizi yalioneesha kutokueleweka kwa dhana ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Wananchi wa Bandakuu walipendekeza kwamba vyama viwili vikuu vya siasa vifutwe na nchi ianzishe serikali isiyotegemea chama chochote. Pia walipendekeza kuviondoa vyama vya upinzani na kurejea katika mfumo wa chama kimoja.

*Jadweli 04: Muhtasari wa matokeo makuu yanayohusiana na SUK*

| Nambari | Hoja zilizoibuliwa |
|---|---|
| **i.** | Dosari za kimuundo/ kutokuwepo kwa SUK katika ngazi za chini za utawala |
| **ii.** | Upendeleo, rushwa, na upendeleo wa kichama katika fursa za ajira za umma |
| **iii.** | Marekebisho ya taratibu za uchaguzi na uhuru wa Tume ya Uchaguzi (ZEC) |
| **iv.** | Kunyimwa haki ya kupata ZanID |
| **v.** | Kubaguliwa na kutengwa kisiasa |
| **vi.** | Umuhimu wa SUK katika kuimarisha mtangamano wa kisiasa |
| **vii.** | Uelewa mdogo kuhusu SUK |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

Kwa kuzingatia idadi ya masuala yaliyoibuliwa katika kila hoja, picha ifuatayo inaeleza asilimia ya uzani wa matokeo makuu:




Kwa kuzingatia idadi ya masuala ambayo wananchi waliyaibua katika kila hoja wakati wa majadiliano, mambo makuu manne yalijitokeza (ambayo yalitajwa kwa angalau 70%) ya hoja zote zilizotolewa na wananchi, nayo ni kama ifuatavyo:

i. Wakati wa mijadala, umuhimu wa SUK katika kuimarisha uthabiti wa kisiasa na kuimarisha uwiano wa kijamii umetajwa mara nyingi zaidi kuliko hoja nyengine yoyote, kwa alama 90%.

ii. Hoja kuhusu kutanua wigo wa muundo wa SUK kufikia ngazi za chini za utawala zimeorodheshwa katika nafasi ya pili, ambapo asilimia 83% wameunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa kufikishwa hadi katika maeneo mengine ya serikali.

iii. Upendeleo na upendeleo wa kisiasa katika ajira za umma unashika nafasi ya tatu kwa asilimia 75%.

iv. Hoja ya kubaguliwa na kutengwa kisiasa inashika nafasi ya nne kwa kuwa na asilimia 70%.

Kwa kumalizia, midahalo iliyofanyika katika majimbo 25 na ile ya Asasi zenye mitazamo sawa na taasisi za serikali ilidhihirisha umuhimu wa kuimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kupanua wigo wake ili kujumuisha miundo ya utawala katika ngazi za chini. Aidha, midahalo hiyo iliangazia baadhi ya vikwazo ambavyo vilitia dosaro kazi iliyokwisha kufanywa. Dosari hizo ni pamoja na kunyima upatikanaji wa ZanID kwa sehemu fulani ya wakazi wa Zanzibar, kuendelea kubaguliwa na kutengwa kisiasa, na upendeleo wa kichama. Ikiwa vikwazo hivi vitaondolewa, SUK hatimaye itaimarika zaidi.

## MAENEO YA VIPAUMBELE VYA KIJAMII NA KIMAENDELEO

Katika kuwasilisha kero zao, wananchi waliibua hoja za ziada mbali na zile zilizobainishwa katika matokeo makuu. Hoja hizi ni pamoja na elimu, huduma za afya, maendeleo ya miundombinu, uelewa wa uchumi wa buluu, kupanda kwa gharama za maisha, rushwa na migogoro ya ardhi, uwezeshaji wa kiuchumi, unyanyasaji wa kijinsia, na ukosefu wa usalama kama inavyoainishwa katika hoja zifuatazo:

### 1. Kuimarisha utoaji wa elimu na vifaa vya elimu

Katika majadiliano mbalimbali, wananchi walieleza masikitiko makubwa kuhusiana na sekta ya elimu, ambayo mengi yalihusiana na ubovu wa miundombinu ya elimu, kama vile uhaba wa madarasa, madawati na viti. Aidha, wananchi walitaja uhaba wa walimu katika skuli za msingi na sekondari, uhaba wa nyenzo za kujifunzia kama vitabu, uhaba wa vifaa saidizi na walimu wenye utaalamu wa kufundisha wanafunzi wenye ulemavu.

#### *i. Uhaba wa walimu*

Wananchi katika majadiliano ya Jongowe, Kojani, Bwejuu, Kilindi na Sizini walieleza kusikitishwa kwao na uhaba wa walimu katika skuli za msingi na sekondari katika Shehia zao. Walidai kuwa idadi iliyopo ya walimu katika skuli hailingani na idadi ya wanafunzi; jambo linalowapa uzito mkubwa wa kazi walimu waliopo katika kutimiza wajibu wao.

Kwa mfano, skuli ya msingi ya Kojani yenye wanafunzi 2,218 ina walimu 27 tu. Hali kama hiyo pia imeelezwa na wananchi kuwepo katika skuli za msingi za Kilindi na Sizini. Kwa mujibu wa mwananchi anayewakilisha walimu, kuna ugumu wa walimu kutimiza wajibu wao kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi jambo ambalo linaleta changamoto kubwa kufikia mafanikio ya elimu.

Katika kijiji cha Matemwe, ambako serikali imepanga walimu katika skuli ya Msingi ya Matemwe, walimu wengi wametumia nafasi hiyo kama hatua ya kuelekea maeneo mengine, hasa ya mijini. Matokeo yake, uwiano wa idadi ya walimu na wanafunzi daima umekuwa chini.

Wananchi wameiomba Serikali ifikirie kuchagua watendaji wenye sifa wanaotoka katika maeneo husika wakati wa kupangia walimu maeneo ya kazi ili kupunguza

suala la kubadilisha maeneo ya kazi jambo linalosababisha upungufu mkubwa wa walimu vijijini.

ii. ***Changamoto zinazohusiana na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu***

Wakati wa mdahalo wa Makadara, wananchi walionesha wasiwasi kuhusu changamoto ya kupata mikopo ya wanafunzi kwa elimu ya juu. Waliitaka serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaostahiki na wenye vigezo vilivyowekwa. Hata hivyo, wananchi walieleza kuwa mikopo ya wanafunzi wakati mwingine inatolewa kwa upendeleo, na wale ambao wana ndugu wa karibu wanaofanya kazi serikalini wanapata mikopo kwa urahisi bila kujali sifa zao.

iii. ***Miundombinu duni ya elimu***

Wananchi walioshiriki majadiliano waliomba kufanyiwa ukarabati wa skuli, kuboresha miundombinu ya skuli na miundombinu ya elimu kwa ujumla. Pia waliomba kuzipatia skuli miundombinu muhimu, ikiwemo ujenzi wa maabara za sayansi na utoaji wa vifaa muhimu vya kujifunzia kama vile vitabu.

Kwa mfano, wananchi katika majadiliano ya Jongowe walidai kuwa hakuna uwiano kati ya madarasa na vyoo vya wanafunzi. Skuli hiyo ina takriban wanafunzi 720 lakini ina madarasa sita tu na vyoo vinne. Hivyo wameiomba serikali kutoa kipaumbele kwa ujenzi wa madarasa zaidi na vyoo katika kuimarisha miundombinu.

Zaidi ya hayo, katika majadiliano ya Fukuchani na Sizini wananchi waliitaka serikali kuboresha mfumo wa elimu na kuhakikisha sera ya elimu bila malipo inatekelezwa kwa kushughulikia masuala ya uhaba wa madawati na walimu sambamba na ukarabati wa majengo ya skuli yaliyochakaa.

iv. ***Uhaba wa vifaa vya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu na walimu wa kufundisha makundi maalum (wanafunzi wenye ulemavu)***

Wananchi katika majadiliano ya Kisauni walibaini upungufu mkubwa wa vifaa saidizi kwa watoto wenye ulemavu na uhaba wa walimu wenye ujuzi unaotakiwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kutokana na changamoto hizo, wazazi wanagoma kuwaandikisha watoto wao skuli wakiamini kuwa kufanya hivyo ni kupoteza fedha, na kuona ni vyema watoto wao wangebaki nyumbani.

Wananchi wa Msuka Mashariki waliripoti kuwa ukosefu wa vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu kama vile viti vya magurudumu, nukta nundu, vifaa vya uchapaji wa maandishi makubwa na vifaa vya kusaidia usikivu, kunasababisha baadhi ya watoto kutohudhuria skuli kama wanavyopaswa.

Wameiomba serikali kuwafundisha walimu stadi maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kuanzisha au kuongeza skuli maalum za wanafunzi wenye ulemavu.

Kwa kuwa wanafunzi wenye ulemavu wanachanganywa pamoja na wanafunzi wengine, wananchi wanaowakilisha walimu wa skuli walipendekeza kuwa serikali inapaswa kuona umuhimu wa kuanzisha skuli maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu.

v. ***Haja ya kuimarisha mafunzo ya amali***

Wananchi wameiomba serikali kuanzisha vituo vya mafunzo ya amali ili kuwajengea uwezo wa vitendo unaohitajika katika ujasiriamali, kuhamasisha vijana kujiajiri badala ya kutegemea ajira serikalini. Vijana wa Uzi na Makangale walieleza kuwa mfumo wa elimu uliopo sasa una mapungufu, ambapo unawaacha wahitimu wengi wakiwa na uelewa wa kinadharia tu na ujuzi mdogo wa vitendo na hivyo kuwaacha katika hali mbaya mara tu wanapomaliza skuli.

*vi.* ***Mapitio ya mitaala kwa kuingiza masomo ya ziada ya ujasiriamali***

Wananchi wa Chwaka, Makadara, Kwagoa, Kojani na Ziwani walieleza kusikitishwa na ongezeko la wahitimu kutoka vyuo mbalimbali ambao wanaoonekana kutokuwa na ujuzi wa kivitendo, na kwa kiasi fulani uelewa wa kinadharia sambamba na kubadilika kwa mtazamo wa wanafunzi wengi kuhusiana utegemezi wa ajira serikalini. Serikali inapaswa kurekebisha mitaala kwa kuingiza mafunzo ya ujasiriamali, uvumbuzi, na programu za kujiajiri, jambo ambalo litaongeza uwezo wa vijana kujiajiri na kupunguza utegemezi wao kwenye ajira za serikali.

*vii.* ***Mapitio ya mitaala kwa ajili ya kuimarisha elimu ya uraia kwa kufundisha katiba ya Zanzibar***

Licha ya kuwa Zanzibar ina katiba na mfumo wake wa elimu, wananchi wa Shengejuu, Matemwe, Chwaka, Ole, Kangagani na Tomondo wana mashaka na ukweli kwamba katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafundishwa katika skuli na inapewa kipaumbele ikilinganishwa na Zanzibar.Walipendekeza kuwa elimu ya uraia iimarishwe kwa kufundisha katiba ya Zanzibar na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika skuli na nje ya skuli ili kuwasaidia Wazanzibari kuielewa vyema nchi yao.

*viii.* ***Changamoto ya walimu wanaojitolea na walimu wa skuli za maandalizi***

Walimu wa kujitolea na waalimu wa skuli za maandalizi ambao wamefundisha kwa muda mrefu wamelalamikia kupuuzwa. Walieleza kuwa baadhi yao wamejitolea kwa muda mrefu, takriban bila ya malipo, bila ya uhakika wa ajira kutoka kwa serikali. Mazingira kama hayo yalielezwa na walimu wa skuli za maandalizi, ambao pia waliomba serikali kuwashirikisha katika mipango ya mishahara ili kuweza kujikimu kimaisha.

*ix.* ***Ukosefu wa maeneo ya kudumu kwa madarasa ya maandalizi***

Wananchi waliipongeza Wizara ya Elimu kwa kuanzisha madarasa ya maandalizi nchini kote. Hata hivyo, mpango huu unakosa msaada wa kuweza kuendesha madarasa hayo katika maeneo ya muda, hivyo wanafunzi kulazimika kuhama kutoka eneo moja hadi jingine. Pia, hali hii inawawia vigumu watoto kuhudhuria skuli, hasa siku za mvua.

Mwananchi wa Sizini alieleza kuwa katika mtaa wake lipo darasa la maandalizi. Hata hivyo, darasa hilo halina mahali pa kudumu au jengo maalum, na hivyo kupelekea kuhama kutoka eneo moja kwenda jingine, hasa katika kipindi cha mvua.

*Jadweli 05: Muhtasari wa hoja za elimu zilizoibuliwa*

| Nambari | Hoja zilizoibuliwa |
|---|---|
| **i.** | Uhaba wa walimu |
| **ii.** | Uhaba wa madarasa, madawati na viti |
| **iii.** | Uhaba wa vifaa saidizi na walimu wenye ujuzi kwa wanafunzi wenye ulemavu |
| **iv.** | Changamoto za upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu |
| **v.** | Kupitiwa upya mitaala na kuongeza masomo yanayohusiana na ujasriamali |
| **vi.** | Kupitiwa upya mitaala na kuweka mkazo katika elimu ya uraia kwa kufundisha katiba ya Zanzibar |
| **vii.** | Walimu wengi wanaopangiwa kazi vijijini kuhamia skuli za mjini |
| **viii.** | Kuchagua watu wenye sifa wanaotoka katika maeneo husika ili kuondosha tatizo la walimu kuhama vijijini |
| **ix.** | Changamoto ya walimu wanaojitolea kwa muda mrefu na walimu wa skuli za maadalizi |
| **x.** | Uhaba wa maeneo ya kudumu kwa skuli za maandalizi |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

2. **Kuimarisha huduma za afya**

Yafuatayo ni masuala yanayohusiana na afya yaliyoibuliwa na wananchi:

i. ***Kuboresha miundombinu ya matibabu (vituo vya afya, hospitali, vifaa vya matibabu na wataalam wa afya)***

Wananchi katika midahalo mingi ya Unguja na Pemba waliitaka serikali kuboresha huduma za afya kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya, vifaa tiba na wataalam wa afya.

Wananchi katika majadiliano ya vijijini walielezea suala la uhaba wa vifaa, ambapo mama wajawazito wanakosa huduma muhimu na za haraka, kama vile uchunguzi wa *ultrasound*, chanjo na wataalam.

Katika midahalo yote iliyofanyika kwenye visiwa vidogo, wananchi waliomba upatikanaji wa huduma kamili ya uzazi; kwa sababu hivi sasa wanajifungulia majumbani na kuhatarisha maisha ya mama na mtoto. Wameeleza ugumu unaojitokeza wakati wa kuvuka bahari kufuata huduma za uzazi katika hospitali za ngambu ya pili.

Wananchi wa Wingwi walieleza shaka yao kuwa shehia yao ina wakazi zaidi ya 3000, lakini bado haina kituo cha afya hali inayowalazimu kufuata huduma katika kituo cha afya kilichopo shehia jirani, ambacho kinategemewa na takriban shehia tano za Jimbo la Wingwi lenye wakazi takriban 12,000 na kusababisha kituo hicho kuelemewa na mizigo mkubwa.

Katika midahalo mingi iliyofanyika vijijini, wananchi walibaini namna uhaba wa madaktari na wataalamu wa afya vituoni unavyosababisha huduma za afya kudorora.

ii. ***Gharama kubwa ya matibabu na mahitaji ya bima ya afya***

Wananchi wa Kisauni, Gulioni, Makadara, Tomondo, na Ijitimai walidai kuwa huduma za matibabu kwa wazee na watu wenye ulemavu ni za gharama kubwa na kwamba serikali haitoi bima ya afya. Wanadai kuwa wazee wengi na watu wenye ulemavu wanateseka kwa kukosa uwezo wa kulipia gharama za matibabu. Wanapendekeza kwamba bima ya afya inapaswa kupatikana kwa wananchi wote.

*Jadweli 06: Muhtasari wa hoja za afya zilizoibuliwa*

| Nambari | Hoja zilizoibuliwa |
|---|---|
| **i.** | Uhaba wa vituo vya afya |
| **ii.** | Uhaba wa madaktari na wataalamu wa tiba |
| **iii.** | Uhaba wa madawa |
| **iv.** | Gharama kubwa za huduma ya afya na haja ya kuwa na bima ya afya |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

### 3. Kuongezeka kwa ufahamu na ushiriki katika uchumi wa buluu

Hoja zilizoelezwa na wananchi kuhusiana na dhana ya uchumi wa buluu ni pamoja na haja ya kuwepo kwa programu zaidi za elimu na uhamasishaji ili kusaidia jamii katika ngazi ya chini kuielewa dhana hiyo. Wananchi pia walizungumzia suala la bei ndogo ya mwani, ukosefu wa zana za kisasa za uvuvi, na haja ya vituo vya mafunzo ili kuwapa Wazanzibari ujuzi unaohitajika kushiriki katika uchumi wa buluu.

Wananchi wa Tumbatu, Kojani, Marumbi, Makoongwe, Ngwachani, Uzi, na Bwejuu waliiomba Serikali kufanya jitihada za ziada katika kutoa elimu na kujenga uelewa kuhusu uchumi wa buluu ambao kwa sasa haueleweki vizuri kwa wananchi walio wengi. Wananchi walishauri kuwe na vipindi vya redio na televisheni kutoa elimu, na serikali inaweza kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kudhamini vipindi hivyo.

Wananchi wa Ngwachani waliongeza kushauri kuwa kwa vile Zanzibar ni nchi ya uchumi wa kutegemea huduma na si ya uchumi wa rasilimali, Wizara ya Elimu inapaswa kuanzisha somo maalumu la uchumi wa buluu katika skuli za sekondari. Wananchi wanaamini kwamba vizazi vijavyo vinapaswa kufahamu zaidi dhana hiyo na kuitumia kukuza uchumi.

**4. Haja ya elimu ya ujasiriamali katika uchumi wa buluu**

***i. Kuanzisha huduma za mafunzo na vituo vya utafiti kwa uchumi wa buluu***

Wananchi wengi wanaonekana kuwa na hamu ya kufahamu dhana ya uchumi wa buluu na wameitaka serikali kuunga mkono ushiriki wa wenyeji na wafanyabiashara katika sekta za uchumi wa buluu. Kwa mfano, wananchi wa Kwagowa waliihimiza serikali kuanzisha warsha na kambi za mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana ili kuwafundisha jinsi ya kutumia fursa za uchumi wa buluu.

Wananchi wa Shengejuu na Kojani walipendekeza kuanzishwa kwa vituo vya mafunzo katika kila Wilaya ya Unguja na Pemba. Kwa kuongezea, wametaka kuwe na kituo cha utafiti makhsusi kwa kazi za uchumi wa buluu. Ujenzi wa taasisi hizo uende sambamba na kutekeleza ajenda ya uchumi wa buluu kwa vile hii itawasaidia Wazanzibari kupata ujuzi unaohitajika na kushiriki kikamilifu katika kuendeleza nchi yao.

Wananchi wa Kojani walipendekeza kuwa badala ya kuhubiri tu kuhusu uchumi wa buluu, serikali inapaswa kutoa mafunzo kwa watu kuhusu mbinu za kisasa za uvuvi, ufugaji wa samaki, na uanzishwaji wa kampuni ndogo ndogo za mazao ya bahari.

***ii. Serikali ifikirie kuongeza thamani ya mwani kwa kutafuta masoko mapya***

Wananchi wa Mchanga Mdogo, Marumbi, Kwagoa, na Bumbwini wameonesha kutoridhishwa na bei ya mwani kwa sasa ambayo ni Tsh 600 kwa kilo moja. Kwa kuzingatia kupanda kwa gharama ya maisha na ugumu wa shughuli ya kilimo cha mwani, bei hii inaonekana kuwa ni ndogo sana. Ikizingatiwa kuwa wakulima wengi wa mwani ni wanawake, serikali inapaswa kuongeza bei na kutafuta masoko mbadala.

Pia, wananchi wa Bwejuu walibainisha kuwa baadhi ya wanunuzi (mawakala) wa zao la mwani ni watu wasioaminika na wamekuwa wadanganyifu katika kuwalipa wakulima. Wananchi waliiomba serikali kuingilia kati na kutafuta masoko mbadala ambayo wakulima au serikali inaweza kuuza moja kwa moja.

### *iii. Uhaba wa vifaa vya kisasa vya uvuvi zikiwemo boti za uvuvi*

Wananchi wa Makoongwe na Kojani wameeleza mahitaji ya vifaa vya kisasa vya uvuvi kama vile boti ziendazo kasi, na kuiomba serikali kuwapatia zana hizo ili kuongeza ufanisi.

*Jadweli 07: Muhutasari wa hoja zilizoibuliwa kuhusu uchumi wa buluu*

| Nambari | Hoja zilizoibuliwa |
|---|---|
| **i.** | Haja ya kuwepo programu za uhamasishaji wa umma juu ya uchumi wa buluu |
| **ii.** | Haja ya elimu ya ujasiriamali kwenye uchumi wa buluu |
| **iii.** | Serikali kufikiria kuongeza thamani ya mwani kwa kutafuta masoko mapya |
| **iv.** | Ukosefu wa vifaa vya kisasa vya uvuvi vikiwemo boti za uvuvi |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*

## 5. Kupanda kwa gharama za maisha

Wananchi wa maeneo ya Wingwi, Maziwa Ng'ombe, Makangale na Mchangamdogo wametoa dukuduku lao kutokana na kupanda kwa gharama za maisha hususan bidhaa za mafuta ya kupikia, sukari na unga. Wamesema kuwa hali hiyo inawasukuma zaidi katika dimwit la umaskini.

Katika midahalo ya Marumbi na Shengejuu wananchi wameeleza hisia zao kuwa kupanda kwa gharama ya mchele kunazidisha ugumu wa maisha ya kila siku kwa Wazanzibari wengi ambao kwao mchele ni bidhaa muhimu. Wananchi wameitaka serikali kuingilia kati kupunguza kodi na ushuru ili bei za bidhaa kwa ujumla zipate kupungua.

## 6. Unyanyasaji wa kijinsia

Kwa mujibu wa wananchi, ingawa serikali imeongeza juhudi zake za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia (GBV), kama vile ubakaji na udhalilishaji wa watoto, matukio hayo bado yanaendelea kutokea. Wananchi wamesema kuwa wahalifu hao wanapaswa kukabiliwa na adhabu kali zaidi za kisheria.

Katika midahalo mingi, wananchi waliiomba serikali iimarishe sheria dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu na kuhakikisha kwamba zinapotokezea kadhia hizo uchunguzi ufanyike kwa haraka, kinyume na utaratibu wa sasa wa ucheleweshaji wa kesi usio wa lazima. Wananchi wamesisitiza kuwa hali ya udhalilishaji wa kijinsia ndani ya jamii ya Zanzibar ni ya kutisha sana na inahitaji umakini wa pekee.

7. **Kuboresha miundombinu na kuhamasisha Uwekezaji wa Serikali katika maeneo ya vijijini.**

Baadhi ya wananchi walieleza hisia zao za kutengwa kiuchumi. Kwa mfano, wananchi wa Uzi Ng'ambwa na Kojani walitoa maoni yao kwamba uongozi wa awamu ya 8 chini ya mfumo wa SUK unapaswa kuweka usawa na umoja kwa watu wote ili waweze kupata haki na fursa sawa. Serikali iwekeze katika maendeleo mijini na vijijini na kujenga masoko bora na ya kisasa ili kunufaisha wananchi kiuchumi.

Wakaazi wa maeneo ya Kisauni na Tomondo walitoa maoni sawa na hayo na kuiomba serikali kuimarisha miundombinu katika maeneo yao. Walieleza kuwa Shehia yao inayozungukwa na Ziwa Maboga, inaathirika kwa kiasi kikubwa na maji ya mvua wakati wa masika, hivyo kusababisha uharibifu wa nyumba kadhaa na kuhatarisha maisha yao. Wakati serikali imetoa ahadi kadhaa za kurekebisha hali hiyo, hakuna kilichotekelezwa.

*Jadweli 08: Muhtasari wa vipaumbele vya hoja za kijamii na kimaendeleo zilizoibuliwa*

| Nambari | Hoja zilizoibuliwa |
|---|---|
| **i.** | Kuboresha utoaji wa elimu na vifaa vya kufundishia |
| **ii.** | Kuimarisha huduma za afya |
| **iii.** | Haja ya elimu zaidi na ushhirikishwaji katika uchumi wa buluu |
| **iv.** | Kupanda kwa gharama za maisha |
| **v.** | Unyanyasaji wa kijinsia |
| **vi.** | Haja ya serikali kuwekeza zaidi katika maeneo ya vijijini |

*Chanzo: Mradi wa Sisi Ni Wamoja; ushirikishwaji wa wananchi uliofanywa na JUWAUZA kati ya Agosti 2021 na Aprili 2022.*




*Uzani wa matokeo katika maeneo mengine ya vipaumbele vya kijamii na maendeleo.*

Kwa kuzingatia idadi ya masuala yaliyoibuliwa na wananchi katika kila hoja wakati wa mazungumzo, hoja tatu kuu ziliibuliwa (ambazo zimejadiliwa kwa zaidi ya asilimia 50%). Hoja hizo ni:

i. Masuala ya kielimu yamezungumzwa mara nyingi zaidi ya hoja nyengine zote wakati wa midahalo, ambayo ilikadiriwa kuwa asilimia 80%

ii. Hoja zinazohusiana na masuala ya kiafya zilichukua nafasi ya pili. Wananchi wengi walitoa maoni yao mbalimbali kuhusu kutatuliwa kwa changamoto za miundombinu ya afya. Maswala ya kiafya yamewasilishwa kwa asilimia 75%.

iii. Uchumi wa buluu na kutengwa kwa maeneo ya vijijini vilichukua nafasi ya tatu na ya nne, kwa asilimia 55% na 50%, mtawalia.

Kwa kumalizia, kutokana na midahalo iliyofanyika katika majimbo 25 ya uchaguzi, hoja zilijikita zaidi katika masuala ya elimu, afya, uchumi wa buluu na haja ya kuongezeka kwa miundombinu ya umma na uwekezaji wa serikali katika maeneo ya vijijini.

## MAPENDEKEZO NA MAONI YA WANANCHI

Wakati wa mazungumzo shirikishi na ya wazi yaliyofanyika wakati wa utekelezaji wa midahalo ya kijamii, wananchi waliweza kueleza matarajio na malengo yao, pamoja na kutoridhika kwao dhidi ya madai yao. Mada ambazo ziliweza au hazikuweza kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na SUK ziliibuliwa kwa sababu midahalo hii ilikuwa wazi kiasi cha kutosha kwa wananchi kueleza hisia zao za ndani. Utawala wa Mheshimiwa Dkt. Mwinyi utanufaika kwa kuyafahamu masuala hayo, kwa vile yanabaki kuwa ni muhimu sana kwa ustawi wa Wazanzibari.

Taarifa hii inaangazia masuala yanayohusiana moja kwa moja na SUK, kama yalivyoelezwa kupitia midahalo ya kijamii. JUWAUZA itafanya kila juhudi kutoa ushauri juu ya masuala haya.

Mapendekezo haya yanatolewa kwa kuzingatia na kuelewa mazingira ya kisiasa hapa nchini. Kwa sababu ya unyeti wake, ambao unahitaji uangalifu na mashauri ya kina, mabadiliko ya kisiasa ya amani na mageuzi yanaweza kuwa ya taratibu sana. JUWAUZA inaamini kwamba iwapo mapendekezo haya yatakubaliwa, yatapelekea mabadiliko makubwa katika kukabiliana na changamoto za miongo kadhaa ambazo zimewasumbua Wazanzibari.

Marekebisho makubwa lazima yafanyike ili kupata suluhisho la muda mrefu na utulivu wa kitaifa, hasa katika wakati huu ambao nchi ipo katika muafaka wa kitaifa na hali nzuri ya utulivu. Wakati ni sasa kwa Zanzibar, kwani utawala wa Mh. Rais Mwinyi unaungwa mkono na umma mkubwa.

Zifuatazo ni mada zinazohusiana na SUK zilizoangaziwa katika majadiliano haya:

1. Muundo uliopo wa SUK hauonekani katika ngazi za chini za utawala, kwani hakuna mifumo iliyowekwa ya SUK katika ngazi hizo.
2. Kuendelea kunyimwa haki ya kupata ZanID kwa baadhi ya Wazanzibari.
3. Umuhimu wa marekebisho ya taratibu za uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuunda Tume Huru ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).
4. Kubaguliwa na kutengwa kisiasa kwa wanajamii mbalimbali.

5. Kurekebisha taratibu za uajiri katika sekta ya umma ili kuzifanya kuwa za haki na uwazi
6. Uelewa duni wa SUK.

**<u>Mtazamo wa Wananchi juu ya Muundo wa sasa wa SUK</u>**

Wakati SUK ikiendelea kufurahia uungwaji mkono mkubwa wa kisiasa wa pande zote mbili, kuna maoni yenye nguvu ya wananchi kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa iko juu kabisa, imejikita kileleni tu kwa ngazi ya utawala (urais na baraza la mawaziri), bila ya kuwepo kimuundo au kiutendaji katika ngazi ya chini ya Serikali. Wananchi walionyesha hisia zao na kueleza yafuatayo:

a) Kwamba ili Serikali ya Umoja wa Kitaifa ifanikiwe kikamilifu na manufaa yake yaonekane na wananchi wa Zanzibar, SUK lazima itanue wigo wa uwepo wake katika ngazi za chini za Serikali (Shehia), ambako ndiko kwenye changamoto nyingi za kiutawala.

b) Kwa kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imejifunga katika ngazi ya urais na uwaziri pekee, uwezo wake wa kutekeleza majukumu na malengo yake daima utakuwa hauna nguvu, jambo ambalo ni hatari.

c) Baadhi ya makundi ndani ya chama tawala (CCM) yanakubali kuwepo muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika ngazi ya juu tu ya Serikali kwa sababu hawana uhakika juu ya athari za kutanua wigo wake.

d) Inafikiriwa kuwa kutanua mamlaka na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hadi ngazi za chini kutavuruga manufaa ya sasa ya kisiasa ambayo CCM inayapata kwa vile kura ziko katika ngazi za chini kabisa ya utawala, na kwamba huko ndiko kwenye ushindani wakati wa uchaguzi hasa katika maeneo ya vijijini.

e) Kwa kuuwacha muundo wa sasa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika ngazi za juu tu, CCM inakuwa katika nafasi nzuri ya kudhibiti michakato ya kisiasa Zanzibar.

**Mapendekezo:**

i. Kutokana na uungwaji mkono mkubwa wa SUK na kuenea kwa umaarufu wa Dkt. Mwinyi, hakuna wakati mzuri zaidi ya sasa wa kutanua muundo wa SUK katika ngazi za chini za serikali. Hivyo, inapendekezwa kwamba SUK ianzishe mchakato wa kutanua mamlaka yake hadi ngazi za chini za serikali.

ii. Vyama vikuu vya siasa vinavyounda SUK vifanye mashauri ya ndani ya kuangalia namna ya kufanikisha suala hili. Jambo hili ni muhimu sana kwani katiba haijamzuia kiongozi kutanua mamlaka yake kiutendaji. Tatizo kubwa katika suala hili ni utashi wa kisiasa ambao ni lazima uzingatiwe, kwa kuwa hilo limo ndani ya uwezo wa wanasiasa.

iii. Kwa kuwa suala hili ni nyeti sana kisiasa, wahusika wanaweza kutanua wigo wa SUK kwa hatua, wakianza na nafasi zisizokuwa na ukakasi mkubwa na kuendelea na zile ambazo ni nyeti zaidi.

iv. Rais anaweza kuunda tume maalum au kikosi kazi ambacho kitakuwa ni shirikishi ili kuongoza mchakato wa uhamasishaji wa kupanua shughuli za SUK hadi ngazi za chini za serikali, kuanzia ngazi ya mkoa na hadi shehia. Kamati hiyo itakuwa ikiripoti moja kwa moja na mara kwa mara kwa Rais, ikisaidiwa na sekretarieti yenye nguvu ya wataalam wenye ujuzi uliothibitishwa katika nyanja zao za utaalamu. Ripoti za kamati hiyo zitasaidia serikali katika kuanzisha kwa haraka utanuzi wa mamlaka ya SUK.

v. Kamati hii pia itapewa jukumu la kufafanua majukumu ya SUK katika kukuza na kuimarisha mchakato wa maridhiano ya kisiasa.

vi. Serikali ishirikiane na iwahuhsishe kikamilifu wadau wengine, wakiwemo wadau wasio wa serikali na wasio wa kisiasa, katika mchakato huu, kwani hao wanaweza kusaidia kwa rasilimali nyengine.

**<u>Kuimarisha upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanziabri Mkaazi (ZanID)</u>**

Kama kuna jambo moja kubwa lililoibua hasira za wananchi wakati wa mijadala ya kijamii, basi ni tuhuma za baadhi ya wanajamii kuendelea kunyimwa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi kutokana na mitazamo yao ya kisiasa.

Baadhi ya wananchi wanaamini kuwa ZanID inatumika kama silaha ya kisiasa, wakieleza wasiwasi wao kuhusu ubaguzi unaowakabili wa kuwa na uhalali wa kupata ZanID na vyeti vya kuzaliwa katika ngazi za Shehia.

Hivyo, ili kutunza heshima ya SUK miongoni mwa Wazanzibari, ni lazima serikali iondoe vikwazo vya kupata ZanID kama ilivyo kwa Kitambulisho cha Taifa (NIDA). Faida za kutoa ZanID kwa wananchi wanaostahiki zinaweza kushinda vitisho vinavyofikiriwa vinavyotokana na wasiwasi wa kisiasa.

**Mapendekezo:**

i. ZCSRA ihakikishe kwamba wananchi wote wanaostahiki wanaweza kujiandikisha na kupata ZanID.

ii. Kukuza ushirikiano kati ya mamlaka ili kuhakikisha ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika mchakato wa usajili wa wapiga kura.

iii. Kuimarisha ushirikiano na wizara zinazohusiana na vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, mashirika yasiyo ya kiserikali, makundi ya dini, na taasisi za kijamii ili kutoa elimu kuhusu umuhimu wa ZanIDs.

iv. Kutoa mafunzo kwa masheha na maafisa wilaya ili kusaidia uelewa wa jamii kuhusu mahitaji na taratibu za usajili ili kupunguza mizozo katika kijamii.

v. Kushajiisha matumizi mazuri ya lugha na na tabia miongoni mwa watendaji wa ZCSRA

vi. Kutumia teknolojia kurahisisha mchakato wa kutuma maombi, kama vile kutumia programu za kidigitali.

**Marekebisho ya taratibu za uchaguzi na uhuru wa Tume ya Uchaguzi**

Kwa hakika, karibu kila serikali duniani kote inakabiliwa na matakwa ya kubadilisha taratibu za uchaguzi. Hii ni kweli hata kwa nchi zilizoendelea. Kikawada, inapokuwepo Tume ya Uchaguzi, basi wito wa kuwa na marekebisho ya tume hiyo yanaendelea kuwepo pia. Kwa hivyo, mawazo haya ya wananchi yanayotokana na majadiliano sio mapya. SUK inafahamu kikamilifu matakwa haya, ambayo pia yamekuwa yakisisitizwa mara kwa mara upande wa Tanzania Bara.

Ingawa madai ya mageuzi ya taratibu za uchaguzi Zanzibar si mapya, bado yanabaki kuwa muhimu kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na serikali nyingine yoyote duniani. Tangu Mapinduzi ya mwaka 1964, Serikali ya Zanzibar imejaribu kufanya mageuzi mengi muhimu, ikiwa ni pamoja na kuunda Baraza la Wawakilishi Januari 14, 1980.

Majaribio kadhaa yamefanywa kuifanyia marekebisho Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Kufuatia mazungumzo ya Muafaka kati ya vyama vya CCM na CUF, Serikali ya Zanzibar ilifanya mageuzi makubwa kwa ZEC ili kuhakikisha uhuru wake na kutopendelea.

Kufuatia muafaka wa mwaka 2001, wajumbe wa pande mbili hizo (CCM na CUF) waliweza kuitumikia ZEC kama Makamishna. Hata hivyo, hii haikupunguza mivutano ndani ya chombo hichi cha kusimamia uchaguzi na miongoni mwa wahusika wakuu wa kisiasa. Wakati uchaguzi ukiendelea kuwa na ushindani mkali, na mara nyingi wenye utata na kupingwa, mivutano bado imeendelea.

Historia inaonesha kuwa mchakato wa uchaguzi Zanzibar bado unabakia ndani ya ZEC. Katika mijadala ya kijamii, ZEC ilishutumiwa kuwa na upendeleo na kukosa uhuru.

ZEC haina budi iendelee kuwepo licha ya changamoto zote hizo. Hata hivyo, ni lazima pia ifanyiwe marekebisho ili kukidhi mahitaji ya msingi ya chombo huru cha uchaguzi kisicho na upendeleo na ambacho utoaji wake wa haki hautapingwa. Sharti kubwa kwa utulivu endelevu wa taifa lenye demokrasia ni usawa na kutopendelea kwa chombo kinachosimamia uchaguzi.

**Mapendekezo:**

i. Kuandaa Kongamano la Kitaifa la Zanzibar la kuangazia maeneo ya mageuzi na michakato ya uchaguzi ili kufikia kiwango kizuri cha ZEC iliyo huru na isiyo na upendeleo.

ii. Kufuatia mapendekezo ya kongamano hilo, Rais afanye marekebisho kwa ZEC kulingana na mapendekezo yatakayopitishwa na kuungwa mkono na Baraza la Wawakilishi kwa kuyatafsiri mapendekezo hayo kuwa sheria zitakazoifanya ZEC kuwa uhuru na kutokuwa na upendeleo.

**Kuondoa Ubaguzi na kutengwa kisiasa**

Majadiliano ya kijamii yamedhihirisha wazi kwamba mafanikio ya kisiasa na kiuchumi ya SUK hayawezi kuonekana na wananchi iwapo wanaona kuwa serikali inawatenga katika maendeleo kwa misingi ya itikadi zao za kisiasa.

Kihistoria, ubaguzi wa kijamii na kiuchumi na kuwatenga baadhi ya watu wa Zanzibar imekuwa ni jambo la muda mrefu na lenye athari inayojikita katika mgawanyiko wa kisiasa. Inaweza kuchukua muda kubadili mwelekeo huo ghafla. Hata hivyo, serikali lazima ianze kuchukua hatua sasa, kwa sababu SUK haitaweza kutimiza malengo yake ikiwa itaendelea kuonekana kuwa inabagua watu wake.

Kwa upande mwingine, kuna malalamiko kuhusu tofauti baina ya mjini na vijijini, ambapo kuna dhana kwamba ustawi wa watu wa vijijini unadunishwa kwa kuwanufaisha wakaazi wa mijini.

Katika hali hii, baadhi ya wananchi walioshiriki majadiliano walikwenda mbali na kudai kwamba hawaoni manufaa yoyote ya kweli ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu inafanana tu na tawala zilizopita.

**Mapendekezo:**

i. Serikali inapaswa kutekeleza sera za kukabiliana na changamoto za kimaendeleo kwa kuelekeza miradi ya maendeleo vijijini na katika visiwa vidogo ili kukuza ustawi wa jamii na kupunguza kukosekana kwa usawa.

ii. SUK ni lazima ishughulikie matatizo yanayowasilishwa na vijana, ambayo yanaweza kuhusisha mbinu bunifu za sera za kiuchumi. SUK inaweza kufikiria kuanzisha mafunzo maalum ya ufundi ili kuwatayarisha vijana kwa kazi au kujiajiri.

iii. Washirika wa maendeleo na wadau wengine wanaoitakia kheri Zanzibar ya sasa na ya baadae wahimizwe kuchangia katika mabadiliko ya sera muhimu za kiuchumi Zanzibar.

**<u>Kurekebisha mfumo wa uajiri katika sekta ya umma</u>**

Sawa na visiwa vingine vyenye uchumi na uwekezaji mdogo wa sekta binafsi, idadi kubwa ya wakazi wa Zanzibar wanaendelea kutegemea ajira za sekta ya umma.

Kwa Zanzibar, ajira katika sekta ya umma hutoa njia salama zaidi za kujikimu. Kwa kuzingatia hili, mtu anaweza kufahamu hisia za wale wanaoamini kwamba fursa za nafasi za ajira katika sekta ya umma haziko wazi na hazitolewi kwa usawa.

Wakati wa majadiliano, wasiwasi juu ya mada hii ulionekana dhahiri. Wananchi walidai kuwa fursa za ajira zinatolewa kwa misingi ya upendeleo, huku wafaidika wakubwa wakiwa ni wale wenye mahusiano na chama tawala.

Walidai kuwa hata uwepo wa SUK haujasaidia kwenye masuala haya, kwani hakuna utofauti. Walidai kuwa kujihusisha na siasa za upinzani ni sababu tosha ya kukosa kila fursa katika ajira za umma.

Walidai kuwa mchakato wa uajiri umejaa "upendeleo," baadhi ya wananchi walibainisha kuwa ubaguzi katika uajiri wa umma unaendeleza migawanyiko ya kisiasa na kubatilisha mafanikio yote yaliyofikiwa na SUK kwa kiasi kikubwa.

Fursa za ajira ni suala la kufa na kupona kila mahali duniani. Isitoshe, uchumi wa Zanzibar kwa sasa ni mdogo mno kuweza kumnufaisha kila mtu.

Hata hivyo, rasilimali kama fursa za ajira zinaweza kugawanywa kwa usawa. Kwa vile ajira ni msingi wa njia ya mtu kujikimu, kukosekana kwake kunaweza kusababisha zahma.

**Mapendekezo:**

i. Badala ya waombaji ajira kutuma maombi kwa njia ya mkono, kuanzishwe mtandao wa kidijitali wa kuajiri ambao utakuwa na jukumu la kusimamia mchakato mzima wa ajira za umma, kuanzia kutuma maombi hadi kupanga orodha fupi ya wasailiwa. Hii inafanana na utaratibu unaotumika Tanzania Bara, ambapo maombi yanachakatwa kupitia mfumo wa kimtandao (Ajira Portal), ambao umesaidia kuboresha ufanisi, uthabiti, na usawa wa mchakato wa ajira za umma.

ii. Ili kuhakikisha kwamba waombaji wanachaguliwa kulingana na sifa na uwezo wao, Tume ya Utumishi Serikalini inapaswa kuwa na umakini zaidi wakati wa kutathmini na kuchunguza maombi ya waombaji.

iii. Mamlaka husika zisimamie kanuni zinazokataza waajiriwa wa serikali waliopangiwa kazi maeneo ya vijijini kuhama kutoka vituo walivyopangiwa kwani kunasababisha upungufu mkubwa wa watumishi vijijini.

iv. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kupata ushauri kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO) nchini Tanzania katika kuandaa taratibu za ajira katika sekta ya umma.

## Kujenga uelewa wa SUK

Kwa kuzingatia umuhimu wa SUK kama chombo cha kuimarisha uhusiano wa kijamii, amani na maendeleo ya taifa, kuna haja ya kuongeza uelewa juu ya mada hiyo. Wananchi wengi wamedai kuwa wanafahamu uwepo wa Serikali ya Umoja

wa Kitaifa huku baadhi wakitarajia kuwepo kwa mfumo huo kutaleta mabadiliko makubwa ikilinganishwa na hali ilivyokuwa awali kabla ya kuanzishwa kwake. Kinyume chake, matarajio mengi bado hayajatimizwa.

Zaidi ya hayo, baadhi ya wananchi wameonesha imani kwamba uwepo wa SUK ni ishara tu, lakini hakujakuwa na dhamira ya kutosha katika kuleta mabadiliko. Lengo zima la uwepo wa serikali limekuwa ni kudhoofisha upinzani tu.

JUWAUZA inaamini kwamba baadhi ya imani hizi zinaendelea kuwepo kwa sababu tu wananchi hawajaelewa ipasavyo masuala muhimu yanayohusiana na SUK, kuwa na matarajio ya kupitiliza, na historia ya kijamii na kisiasa ya Zanzibar. Wananchi lazima wafahamishwe kuhusu kitu gani kinaunda SUK, mantiki na msingi wake, na jinsi inavyoweza kuwa daraja zuri la kutatua mizozo ya kisiasa na kuimarisha mahusiano ya kijamii na kitaifa.

Serikali, kwa kushirikiana na asasi za kiraia, haina budi kuwaelimisha wananchi juu ya wajibu wao katika kudumisha mtangamano wa kitaifa. Ufahamu huu unaweza kutumika kama nyenzo muhimu kwa wananchi kuepuka shinikizo lolote la kiitikadi au kisiasa, au kitu kingine chochote kinachoweza kuzuia kufikiwa kwa hatua muhimu.

**Mapendekezo:**

i. Kuandaa kampeni ya SUK ya kuongeza uhamasishaji itakayofanyika kupitia majadiliano ya kijamii au midahalo itakayofanyika katika ngazi ya shehia nchini kote.

ii. Elimu ya uraia katika skuli za msingi na sekondari inapaswa kutiliwa mkazo, kwa kuingiza katika mitaala masomo makhsusi juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na umuhimu wa kuhifadhi umoja kwa ustawi wa Zanzibar na vizazi vijavyo.

iii. Wizara ya Elimu ianzishe vilabu vya Umoja na Mshikamano katika skuli za msingi na sekondari Zanzibar ili kufundisha kizazi kipya umuhimu wa kudumisha umoja na mshikamano kwa kwa lengo la kuishi kwa amani.

## HITIMISHO

Wazanzibari kutoka majimbo mengi yaliyoshirikishwa katika mradi huu ni waumini wakubwa wa SUK. Ili kuzuia mivutano ya kisiasa kuibuka tena, ni muhimu kuhamasisha SUK miongoni mwa wananchi, vyama vya siasa, na wadau wengine kwa ajili ya kukuza ari ya ushirikiano, umoja na maridhiano.

Baadhi ya wananchi wanaendelea kukumbana na changamoto za kutengwa na kubaguliwa kisiasa, kama vile kunyimwa haki ya kupata ZanID, upendeleo wa kisiasa katika mchakato wa ajira za umma, na ugawaji usio na uwiano wa miradi ya maendeleo katika maeneo kulingana na tofauti za kisiasa. Changamoto hizi zikipuuzwa, zinaweza kuzua mivutano ya kisiasa na kuzorotesha juhudi za upatanishi. Wahusika lazima waikabili hali hiyo kwa tahadhari kubwa.

JUWAUZA inaunga mkono SUK na iko tayari kushirikiana kwa karibu na serikali na wananchi kwa ujumla. Tunaamini umoja ndio ufunguo wa mafanikio, na tuna matumaini makubwa kwamba serikali itachukua juhudi zinazohitajika ili kuondokana na vikwazo vilivyoainishwa ili kufikia umoja wenye nguvu, ustawi, utu, amani na mshikamano. Tuna ari na uwezo wa kushirikiana na serikali au mtu mwingine yeyote mwenye nia sawa na yetu ili kuwezesha utekelezaji wa hatua zilizopendekezwa.

Wananchi lazima wawe na matumaini na kustahamiliana baina yao. Wanapaswa kuamini kwamba serikali yao inawajibika na itafanya kila jitihada kutatua matatizo yao.

Kama inayotetea watu wenye ulemavu na wanawake, tunaamini kwa dhati kwamba kuishi pamoja kwa amani kutapunguza uwezekano wa mizozo ya kijamii na kuimarisha umoja wetu.

**Tunaiomba Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuzingatia mapendekezo yetu yanayotokana na maoni ya wananchi katika kukabiliana na kero zao na tuko tayari kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano kwa ajili ya kuboresha jamii yetu ya Kizanzibari.**

+255 773 222 466 / +255777878293
Fax: 024 2235135 info@juwauza.or.tz
1731, Kikwajuni - Zanzibar www.juwauza.or.tz